



## Hawezi kuwa na imani mmoja wenu mpaka ampendeleee ndugu yake anachokipenda yeye katika nafsi yake

Kutoka kwa Anasi bin Maliki -radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Hawezi kuwa na imani mmoja wenu mpaka ampendeleee ndugu yake anachokipenda yeye katika nafsi yake".

[صحيح] [متفق عليه]

Amebainisha wazi Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa imani kamili ya Muislamu yeyote haikamiliki mpaka ampendeleee nduguye anachokipenda yeye, katika matendo mema, na aina mbalimbali za wema katika dini na dunia, na achukie kwake kinachochukiwa na nafsi yake, na ikiwa ataona kwa ndugu yake Muislamu kuna upungufu katika dini yake, basi ajitahidi kurekebisha, na akiona kuna jambo la kheri basi amtie moyo na amsaidie, na amnasih katika dini yake au mambo ya dunia yake.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4717>

